

Mungu wangu, kwa nini umeniacha

Sikukuu ya Matawi
♩ = 77

Zaburi 21, 89, 17, 18a, 19, 20; 23, 24a

Musique et Harmonie: Gloire VINCENT

S
A
T
B

Mu - ngu wa - ngu, Mu - ngu wa - ngu, kwa ni - ni u - me - ni - a - cha?
Mu-ngu wa-ngu, Mu-ngu

8

1. Wote wanaoniona wanicheka,
wanacheka na kutikisa kichwa;
"Alimwamini Bwana, naye amwokoe,
amwopoe, kwani anampenda!

2. Kwa maana mbwa wengi wamenizunguka,
kundi la waovu wananisonga:
wamenitobowa mikono na miguu,
naweza kuhesabu mifupa yangu yote.

3. Wanagawanya nguo zangu kati yao,
wanaipigia kura kanzu yangu.
Nawe, ee Bwana, usisimame mbali !
Ewe Bwana msaada wangu, fanya haraka kunisaidia!